



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

RUHUSA KWA MABASI YA DAR – MTWARA KUPITA KWA DHARURA SONGEA - MAKAMBAKO – IRINGA

Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini, inasikitika kutangaza kuwa, kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha mikoa ya Kusini – Mashariki mwa Tanzania, kumekuwa na uharibifu mkubwa wa barabara inayotoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Lindi na Mtwara kupitia Kilwa, katika maeneo ya Somanga, Njia nne, Masaninga, Cheketu na Matandu, ambapo barabara hiyo kwa sasa haipitiki kabisa.

Kutokana na changamoto hiyo, Mamlaka inaendelea kushirikiana na wasafirishaji na Jeshi la Polisi ili abiria walioshindwa kuendelea na safari warudishwe katika vituo walivyoanzia safari. **Aidha, mamlaka inatoa ruhusa ya dharura kwa wasafirishaji ambao ratiba zao zimeathirika na uharibifu huo, kutumia njia mbadala kwenda na kurudi Dar es Salaam - Lindi/ Mtwara kupitia Songea, Makambako na Iringa mpaka barabara iliyoharibika itakapoanza kutumika.**

Rai inatolewa kwa madereva watakaopita njia ambazo hawana uzoefu nazo, wachukue tahadhari zaidi, hususan, wanapopita maeneo yenye miteremko au milima na wasipitishie mabasi katika barabara zilizojaa maji. Katika njia hizo mbadala, wasafirishaji wazingatie viwango vya nauli kulingana na umbali kama vinavyooneshwa katika majedwali ya nauli elekezi zilizotolewa na LATRA.

Mamlaka inawakumbusha watoa huduma wote kuzingatia Sheria na Kanuni za huduma wanazotoa, ikiwemo kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao. Watoa huduma za tiketi mtandao wanatakiwa kutoa ushirikiano wa haraka kwa wasafirishaji kutokana na mabadiliko haya ya njia.

Abiria wanakumbushwa kutoa taarifa za changamoto za usafiri kwa kupiga simu bila malipo namba 0800110019/20 inayofanya kazi siku zote saa 24.

Salum Pazy
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano